MADA NA. 1 – Ushiriki wa Wananchi Katika Michakato ya Utekelezaji wa Programu za MKUKUTA/MKUZA. Mafanikio na Changamoto.

1.1 Utangulizi

Mraghibishi wa Mada, Bw. Jeff Makongo alisema lengo la mada hii ni kubadilishana mawazo kuhusu MKUKUTA/MKUZA. Tunataka tujue MKUKUTA/MKUZA ni nini, umefanya nini kwetu na tunasherehekea nini? Wachokoza Mada mbalimbali watatupa uzoefu wao kama waandaaji wa programu hizi, na hatimaye tuweze kuziboresha tunapoingia awamu ya pili (ya kwanza ni 2005 – 2010).

Maswali ambayo yataongoza mada na mjadala wetu ni kama ifuatavyo:

- Ni wangapi miongoni mwenu wanaweza kuuelezea MKUKUTA kwa ufasaha zaidi ?
- Wananchi wanapenda kufahamu tunapozungumzia MKUKUTA/MKUZA tunamaanisha nini?
- Tangu programu hizi zimeanza, wadau mbalimbali wameshiriki kwa namna gani katika maandalizi?
- Wadau waliopo hapa wameshiriki kwa namna gani katika utekelezaji au kupima matokeo.
- Tunayo maeneo katika programu hizi ambayo tunajidai tumefanya vizuri. Je, ni maeneo gani tungeweza kufanya tofauti tunapoingia awamu ya tatu?

1.2 *Wasilisho kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, Zanzibar-* Dk. Hemed Rashid Hikmany

Historia fupi ya MKUZA inaanzia miaka ya 1980 ambapo SMZ ilibaini kuwa hali ya maendeleo ya watu kijamii na kiuchumi ilikuwa ikishuka, na ilionekana umasikini haupungui. Mwaka 1990 – 1993 uliandaliwa mpango kujaribu kuzaa mipango ya kuwawezesha wananchi wazalishe mali na kutengeneza ajira, lakini dhana hii ilionekana nyembamba sana.

Dira 2020 ilikuwa na malengo ya kuinua uchumi na kumsaidia mwananchi kuondokana na umasikini. Pato la taifa (GDP) linaweza kuwa kubwa lakini mwananchi akaendelea kuwa mnyonge kiuchumi. Hali hii ndiyo iliyozaa MKUZA mwaka 2005, programu iliyolenga sekta ya elimu, afya, kilimo na ukuaji wa uchumi.

Dhana hii ilionekana finyu na mwaka 2006 ikafanyiwa mapitio na MKUZA ulipoandaliwa lengo kuu likawa ni kukuza uchumi wa nchi na wa mwananchi.

Wananchi walishiriki katika kuandaa mpango huu na pia katika mapitio. Ushirikishwaji wa wananchi ulifanyika kwa njia ya demokrasia-wakilishi. Jumuia mbalimbali ziliteua washiriki katika ngazi mbalimbali mwaka 2005 – 2007. Walioshiriki ilijumujisha wanafunzi, wananchi ngazi za Shehia, Wilaya, makundi maalumu, n.k. Pia watu wanaoishi maeneo ya mbali kusiko miundombinu na wafanyakazi maalumu – wavuvi, wakulima, wakwezi, n.k.

Changamoto za MKUZA ni pamoja na kwamba vipaumbele viko vingi kwa makundi mbalimbali; ufinyu wa rasilimali, nyingine hazipo kabisa. Katika mpango wa sasa vifo

vya watoto vimepungua kwa kiasi kikubwa, wakati vifo vya kina mama bado ni changamoto. Vituo vya afya havitoshi, elimu ya wakina mama bado ni duni. Idadi ya wasichana wanaosoma masomo ya sayansi imeongezeka.
Uchambuzi wa matatizo unafanyika kwanza na baada ya hapo unatafuta mbinu za kushughulikia tatizo hilo. Wakati wa kuandaa mkakati mpya, unaangalia viashiria vilivyowekwa, vipi vimetekelezwa na vipi vimebaki. Yale yaliyofanywa vizuri (k.m. uandikishaji wa watoto katika shule) yafanywe kuwa endelevu.
Mwisho AZAKi zina wajibu wa kutengeneza taratibu za kusaidia programu hizi.

***1.3 Mchango kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi* – Bw. Cheyo**
MKUKUTA maana yake ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania. Mkakati huu ni mwendelezo wa juhudi tulizoanza tangu Uhuru, mwaka 1961 tunapopambana na maadui watatu – Umasikini, Ujinga na Maradhi. Juhudi hizi zilizaa mabadiliko mengi ya kisekta. Katika MKUKUTA, mikakati yote inawekwa kwa pamoja (Afya, Elimu, Kilimo, Maji, Utawala Bora, n.k.)
Kimsingi MKUKUTA/MKUZA unalenga maeneo makuu matatu:

- Ukuaji wa uchumi
- Ustawi na Maendeleo ya Jamii (Elimu, Afya, Maji, Makundi yaliyo pembezoni, Watoto, Wanawake, n.k.)
- Uwajibikaji na Utawala Bora – ili kufanikisha yote hayo utawala bora ni muhimu.

Dira ya Maendeleo (Vision 2025) ya taifa ni nchi yetu ifikapo 2025 iwe na maendeleo ya kati na iwe na jamii isiyokuwa na umasikini (Poverty-free society)

Je, katika MKUKUTA wadau mbalimbali walishiriki vipi?

- Katika hatua za maandalizi – iliyopata umiliki wa wananchi, serikali ilitoa mwongozo na kuandaa mkakati. Taasisi mbalimbali zilialikwa ili kutoa maoni ya jinsi ya kushirikisha wananchi. Kwa hiyo Bunge, AZAKi, ALAT, n.k. walialikwa.
- Maoni yalikusanywa na Sekretarieti
- Rasimu ilitayarishwa na kurudishwa kwa taasisi mbalimbali ili kujadiliwa upya hadi kukubalika.

MKUKUTA unaeleza majukumu ya kila mshiriki – Wafadhili, AZAKi, Serikali Kuu na serikali za mitaa hadi kwa wananchi.
Changamoto za MKUKUTA ni pamoja na:

- Pamoja na kupiga hatua katika baadhi ya maeneo kama vile kupungua kwa vifo vya watoto, uandikishaji watoto mashuleni, vyuo vikuu, maji; kasi ya ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja bado ni ndogo mno, wastani wa asilimia 2 hadi 2.5 tu! Uchumi unakua (asimia 6), lakini watu bado wanaendelea kuwa masikini. Sekta ya Kilimo lazima ipewe kipaumbele kwa sababu ndiyo ajira ya Watanzania wengi, zaidi ya asilimia 70.
- Makundi yaliyopo pembezoni ndiyo yanayoongoza kwa umasikini (walemavu, yatima, wajane, n.k.) na hawa wapewe uangalizi maalumu.

***1.4 Maoni kutoka ANGOZA* – Bw. Hassan Khamis Juma**

Baada ya Dira 2020, MKUZA uliandaliwa kama programu ya muda wa kati. Katika kuandaa MKUZA wadau wakubwa kwa kiasi fulani walishirikishwa na tunaweza kusema kulikuwa na umiliki wa wananchi. Pamoja na ANGOZA kupewa nafasi mbili, tunadhani ushiriki wa AZAKi ungekuwa mkubwa zaidi na serikali isiwe na nafasi kubwa.
Katika utekelezaji wa MKUZA, imeonekana uelewa wa elimu ya uraia kwa wananchi ni mdogo sana. Wadau waliopo wajengewe uwezo.
MKUZA unalenga maeneo makuu mawili:

- Umasikini wa kipato – hii ni ajira au shughuli ya kuingiza kipato
- Umasikini usio wa kipato – elimu, afya, maji, n.k.

Katika kutekeleza dhana ya MKUZA, bado suala la kupeleka madaraka mikoani halijatekelezwa. Pia ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma (PPP) bado unalegalega. Sera ya AZISE Zanzibar imeshapitishwa na Bunge lakini utekelezaji wake haujaanza.

AZAKi zina wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kufanya tathmini ya upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi (Participatory Public Service Delivery Evaluation) (maji, hospitali, shule) na pia PETS. Wananchi washirikishwe.

***1.5 Uzoefu kutoka Policy Forum* – Bw. Ibrahim Ugulumu**
Sehemu zetu mbili za Muungano zinaongozwa na Dira za Maendeleo, kwa Zanzibar kuna Dira ya Maendeleo (Vision) 2020, wakati Tanzania Bara ni Vision 2025. Hizi zinatoa picha ya nchi iweje ifikapo 2020/2025. Dira hizi zinaendana na mipango ya wakati husika. Mwanzoni ilikuwa ni mipango ya muda mfupi. Dira 2020/2025 ni mipango ya muda wa kati. Kila mwaka mapitio hufanyika kuona iwapo tupo katika njia sahihi hatupotezi dira. Katika hili, mchakato wa kufanya mapitio hauna budi kufanywa na wadau (AZAKi, n.k.), kazi ya Serikali ni kutoa miongozo.
Mambo makuu ya kuzingatia ni:

- Umiliki wa mkakati uwe wa wananchi, wananchi waone mkakati unaotayarishwa ni wao. Hili linawezekana kwa kutumia magazeti, vipeperushi, majadiliano, tovuti na hata wananchi waliopo nje ya nchi.
- Matatizo ya wananchi yapewe kipaumbele – hasa upatikanaji wa huduma za kijamii.

Baada ya duru za majadiliano ilionekana kwamba ***wananchi hawataki sekta za kipaumbele bali wanataka matokeo ya kipaumbele.*** Maeneo matatu yaliyoainishwa katika MKUKUTA/MKUZA ni:

- Kukuza uchumi - kilimo, ufugaji, uvuvi n.k.
- Kukuza sekta za huduma za jamii – elimu, afya, maji, n.k.
- Utawala bora – hili ni sharti muhimu (pre-requisite) ya kupata mafanikio katika klasta hizo mbili

Utekelezaji: AZAKi zimekuwa na mchango katika maeneo yote hayo matatu hapo juu, lakini zinakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo upatikanaji wa mitaji au rasilimali, na hata ikipatikana haitoshelezi mahitaji.

- Changamoto nyingine za utekelezaji ni miundombinu ambayo inachangia kudumaza shughuli zote za kiuchumi na kijamii
- Mahusiano ya AZAKi ngazi ya kitaifa ni mazuri zaidi na Serikali kuu kuliko mahusiano ya asasi katika ngazi za chini na halmashauri. Katika hali hii, mipango inayopangwa katika ngazi ya halmashauri aghalabu kuwahusisha wananchi.

Ufuatiliaji: AZAKi nyingi zimekosa utaalamu wa ufuatiliaji (PETS). AZAKi zinatakiwa kusoma taarifa za maendeleo za maeneo yao ili kuweza kuzifuatilia. Moja ya wajibu mkubwa wa AZAKi ni kinga kwa wanajamii walioko katika mazingira magumu na hatarishi, k.m. watoto yatima, wajane, walemavu, wazee, n.k. Changamoto ni nyingi lakini hasa ufinyu wa rasilimali.

Mwisho tusisahau Utamaduni wa Mtanzania. Tutakutambuaje kuwa wewe ni Mtanzania? – ni kwa vyombo vya asilia, chakula asilia, ngoma n.k.

Huu ni wakati muafaka wa kuchangia katika MKUKUTA /MKUZA wa hatua inayofuata kwani Serikali ndio inafanya mapitio.

1.6 Mjadala wa Pamoja, Maoni na Mapendekezo

Ufuatiliaji na tathmini. Kuna taratibu gani katika ngazi ya kitaifa na ngazi za chini kufanya ufuatiliaji na tathmini ya MKUKUTA/MKUZA?

- Kitaifa kuna muundo wa kuonana na wataalamu na katika ngazi za chini kuna utaratibu uliowekwa na TAMISEMI

Serikali haiko tayari kukubali matokeo ya ufuatiliaji. Serikali inabidi ielewe kwamba AZAKi zinaingia kwenye mgongano na watendaji.

- Serikali inajitahidi kupokea maoni na si kwamba inakataa taarifa kutoka asasi mbalimbali. Kama kuna mapungufu, basi hizi ni changamoto.
- Ushiriki wa AZAKi katika kufanya Ufuatiliaji ni dhaifu. Katika Wiki ya Sera ya Umasikini *(Poverty Policy Week)* ni muda muafaka kwa AZAKi kutoa maoni na ufuatiliaji wake. Hadi sasa hakuna mfumo rasmi wa ufuatiliaji na kutoa mrejesho. Hii pia ni changamoto kwa The Foundation na asasi nyingine.

Makundi Maalumu: Serikali ilitamka kwamba makundi haya yaliyo pembezoni yamechelewa kuingizwa kwenye MKUKUTA. Je, sasa yataingiaje, hasa Maalbino? Pia ukiangalia takwimu za msaada inaoutoa Serikali kwa makundi haya inasikitisha, imesaidia watoto 270 tu nchi nzima!

- Makundi maalumu yataingia katika awamu ya pili ya MKUKUTA. Tunachotakiwa ni kupata maoni, Serikali iko tayari kutoa hifadhi ya jamii *(Social Protection).* Kila kundi la watu wenye mahitaji lina mahitaji yake mahususi na Serikali inajaribu kuainisha mahitaji hayo.

Ufafanuzi wa Ukuaji wa Uchumi na Hali za Wananchi

- Ili kuinua hali ya wananchi ni kuongeza kipato na kuongeza ajira nzuri na huduma za jamii. Sekta ya Kilimo imekuwa haikui kama inavyostahili hivyo kipato cha wananchi wengi kutoongezeka. Kwa huduma za jamii zimeendelea kuboreka.

Changamoto:

- Dhana ya MKUKUTA/MKUZA bado haijasambazwa na kueleweka vyema na wananchi.
- Mawasiliano – taarifa zitawafikiaje wananchi ili washiriki na pia wapate mrejesho. Na baada ya kongamano, nini kitafanyika? Pawepo na mfumo mahususi wa kufanya ufuatiliaji na kupeana taarifa
- MKUZA – Kuna matrekta mawili tu Pemba nzima, moja bovu!
- Masheha wasio waaminifu wanachangia kuzorotesha MKUZA, hawa wanastahili kupewa elimu ya uraia

Mapendekezo:

- Taasisi za Serikali zinazoandaa sera zikae na AZAKi, uwakilishi wa wananchi uwe mpana zaidi, wawakilishi wa AZAKi na jumuia nyingine za kijamii waongezeke katika kamati hizi.
- Asasi za Kiraia zijengewe uwezo ili ziweze kutekeleza PETS na programu nyingine kwa niaba ya wananchi.
- Mataifa yanayosababisha hewa ya ukaa yawajibishwe.
- Tuangalie jinsi ya kuwashirikisha watu wenye ulemavu hasa wasioona na viziwi katika shughuli za kupanga maendeleo